**NAMBA 10: MARKO 15:1–39: MSALABA**

Hebu turejee kwenye kitabu cha **Marko sura ya kumi na tano** – na kwa pamoja tutasoma **mstari wa kwanza hadi thelathini na tisa**. Hii ni sura ya muhimu sana katika injili ya Marko, kwa sababu inatueleza kuhusu kifo cha Yesu msalabani. Na tunaposoma kuhusu kusulubiwa, inatupasa tukumbuke kwamba, ingawa tukio hili lilitokea zaidi ya **miaka elfu mbili** iliyopita, bado ni tukio muhimu sana katika historia yote – na ni tukio ambalo linatuathiri mimi na wewe. Na hii ndio imani ya Kikristo. Hebu tusome sasa. **Marko sura ya kumi na tano, mstari wa kwanza hadi thelathini na tisa**.

Kabla tujifunza kuhusu kusulubiwa na kifo cha Yesu, kuna maswali tatu nataka kuuliza. **Namba moja**. Pilato alikuwa ni nani? **Namba mbili**. Baraba alikuwa ni nani? **Namba tatu**. Simoni Mkrene alikuwa ni nani? Watu hawa ni akina nani? Na wanafanya nini katika habari hii? Kwanza, **Pontio Pilato**, yeye alikuwa ni nani? Kwa kweli, hatujui chochote kuhusu maisha yake, kabla ya kuwa Gavana wa Yudea. Hakuna taarifa yoyote. Tunaweza kudhania kuwa alikuwa ni mtu msomi na tajiri, na ya kwamba alikuwa kiongozi katika jeshi la Kirumi, lakini hatujui kwa uhakika; Bibilia haituambii chochote. Tunajua kwamba alikuwa Gavana wa Yuda kwa **miaka kumi** hivi – kuna baadhi ya kumbukumbu za kihistoria, ambazo zinatueleza hivyo. Watawala wa Kirumi walikuwa wamemweka yeye kuwa kiongozi katika sehemu hii ya Israeli; yaani Yuda.

Pia tunajua kuwa alikuwa ameoa. Marko hatuambii habari hii, lakini injili ya **Mathayo** inatuambia hivyo. Katika **Mathayo sura ya ishirini ya saba, mstari wa kumi na tisa** tunaambiwa kuwa, mke wa Pilato aliota ndoto kumhusu Yesu, kabla tu ya jaribu hili. Alituma ujumbe kwa mume wake Pilato akisema: "*usiwe na jambo lolote juu ya mtu huyu asiye na hatia*". Tunalolijua kwamba aliupuuzia ushauri wake. Pilato hakuwa na umaarufu miongoni mwa Wayahudi. Alikuwa amewatukana na kuwakosea kwa mara nyingi. Alikuwa ameiba fedha kutoka hekaluni, na matendo yake nayo yalikuwa yamesababisha ghasia miongoni mwa watu wa Yerusalemu. Miaka michache tu baada ya habari hii katika **Marko sura ya kumi na tano**, Pilato alifukuzwa kazi na mkuu wake, kwa kuwa kiongozi mbaya. Baadhi ya taarifa zinasema kuwa alijiua kwa sababu aliona aibu ya kupoteza kazi yake.

Huyu ni mtu, Pontio Pilato, ambaye alikuwa na mamlaka ya kuamua kama Yesu aishi au afe. Kumbuka, kwa sababu Warumi walikuwa ndio watawala, viongozi wa Kiyahudi hawakuwa na mamlaka ya kumuua mtu. Hawakuweza kuweka adhabu ya kifo; ni Gavana tu wa Kirumi aliyeweza kufanya hivyo.

Na hivyo tunaona katika **mstari wa kwanza** kwamba walimpeleka Yesu kwa Pilato, na walimwomba amhukumu Yesu. Je, Pilato anamwambia nini Yesu katika **mstari wa pili**? "*Je, wewe ni Wafalme wa Wayahudi*"? Mafarisayo walimshutumu Yesu kwa kukufuru, lakini pia walikuwa wamemwambia Pilato kwamba, Yesu alikuwa amejiita Mfalme wa Wayahudi. Pilato hakujali kuhusu kukufuru. Wayahudi walijali sana hilo, lakini Pilato hakujali. Hata hivyo, mara zote Pilato alikuwa akifuatilia kama mtu alidai kuwa yeye ni mfalme. Hilo lilikuwa ni tishio kwa mamlaka ya Kirumi. "*Je, wewe ni Wafalme wa Wayahudi?*", alimwuliza Yesu. Na jibu la Yesu ni fupi sana: "*Ndiyo mimi ndiye*". Maneno matatu tu – ndiyo aliyoyasema. Ni maneno haya tu ya Yesu ambayo Marko aliyaandika katika jaribio hili. **Mstari wa tatu** unatuambia kuwa makuhani wakuu walimshutaki Yesu kwa mambo mengi - lakini Yesu alinyamaza kimya. Pilato hakuweza kuelewa kwa nini Yesu hakujitetea mwenyewe. Angalia katika **mstari wa tano**: "*Yesu hakujibu, na Pilato alishangaa*".

Kuna mstari katika Agano la Kale ambao unasema kitu kile kile kimoja kumhusu Yesu. Turejee katika Kitabu cha **Isaya, sura ya hamsini na tatu, mstari wa saba**. Kitabu cha Isaya kiliandikwa **miaka mia saba** kabla Yesu kuzaliwa – na bado kifungu hiki katika **sura ya hamsini na tatu** kinaeleza kwa kweli juu ya kile kilicho-tendeka msalabani. **Mstari wa saba** unasema hivi: "*Alionewa, lakini aliyenyekea, wala hakufunua kinywa chake; kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, na kama vile kondoo anyamazayo mbele yao wakatao manyoya yake; naam, hakufunua kinywa chake*". Na hapa katika **Marko sura ya kumi na tano, mstari wa tano** unabii wa Isaya unathibitika kuwa kweli. "*Yesu bado hakujibu*". Wala hakujitetea mwenyewe.

Na kisha tunapokuja katika swali letu la pili tunajiuliza: Baraba alikuwa ni nani? Angalia katika **mstari wa saba**. "*Mtu mmoja aitwaye Baraba alikuwa amefungwa gerezani, pamoja na waasi wengine kwa kuwa walikuwa wamefanya mauaji katika uasi*". Huyu alikuwa ni mhalifu hatari, ambaye alikuwa gerezani. Alikuwa gaidi wa Kiyahudi, ambaye alikuwa amejihusisha na vurugu, na watu walikuwa wameuawa kwa sababu yake. Lakini hapa kuna hatu inayofurahisha. Jina Baraba linamaanisha nini? Tenganisha jina lake katika maneno mawili. Bar - Abba. Neno '*Abba*' lina maana gani? Umeshalisikia kabla katika Biblia. Katika lugha ya Kiyahudi maana yake 'Baba' - Abba. Na neno '*bar*' maana yake ni *'mwana wa*'. Kwa hiyo, jina lake linamaanisha '*mwana wa Baba*'. Umati watu ulikuwa ukipiga kelele, kuomba mharifu hatari aachiliwe huru, ambaye jina lake ni '*mwana wa Baba*'. Na walimwomba Pilato amsulubishe Yesu, Mwana wa Baba. Walikuwa na jina moja (Yesu na Baraba) – lakini mmoja alikuwa ni mtu mwovu, ambaye alikuwa ametenda dhambi nyingi, na mwingine, Mwana wa Mungu Baba, alikuwa mkamilifu na hakuwa amefanya makosa yoyote. Huo ndio ujumbe wa msalaba, sivyo? Mtu mwenye dhambi ambaye alikuwa ametenda makosa, aliachiliwa huru na kusamehewa, ingawa alikuwa hastahili. Lakini mtu mkamilifu Yesu, Mwana wa Mungu, ambaye hakustahili kufa, alipelekwa msalabani. Kwa sababu ya Yesu, Baraba aliwekwa huru. Ni sawa na ilivyo kwetu. Tunastahili kufa kwa sababu ya dhambi zetu - lakini Yesu alikuja ulimwenguni kuchukua nafasi yetu, ili tuweze kuachiliwa huru kutoka gereza la jehanamu, na kuwa na uhuru.

Je, unaweza kuona uhusiano wetu sisi na Baraba? Unaweza kusema kwamba wewe si mwovu kama Baraba alivyokuwa, lakini wewe bado ni mwenye dhambi. Sisi sote tumefanya makosa. Sote tumetenda dhambi. Nawezaje kujua hayo? Ni kwa sababu Biblia inaniambia! Katika **Warumi sura ya tatu, mstari wa ishirini na tatu** inasema kwamba, "*wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu*". Mtu mwovu Baraba ni aliachiliwa huru – ingawa hakustahili, na badala yake, Yesu anaadhibiwa. Kama wewe ni Mkristo, ujue kuwa wewe umekuwa huru; wewe umesamehewa dhambi zako, na badala yake, Yesu amechukua adhabu yako, ingawa yeye hakufanya uhalifu, na wala hakuwa mwenye dhambi! Hii ni picha yenye nguvu, sivyo?

Pia inashangaza tunaposoma kwamba, Pilato hakutaka kumsulubisha Yesu. Alijua kwamba Yesu alikuwa hajatenda uhalifu wowote, na hivyo alijaribu kumwokoa Yesu kutoka msalabani. Angalia **mstari wa kumi na nne**: "*Ni kosa gani ametenda*"? Yeye pia anapendekeza kwamba, Yesu ataadhibiwa na kisha atachiliwa huru - lakini umati haukutaka hivyo. Hatimaye, Pilato alimtoa na kukubaliana na madai yao. Angalia katika **mstari wa kumi na tano**: "*kwa kutaka kuuridhisha umati, Pilato alimwachilia Baraba. Alimtoa Yesu apigwe viboko, na kasha akamkabidhi ili asulubiwe*". Na hii inatuonyesha nini kuhusu Pilato? Alikuwa kiongozi dhaifu ambaye alikuwa na hofu ya watu, na hivyo akawapa kile walichotaka, ili kwamba wasisababishe shida yoyote kwake. Huyu ni mtu ambaye alijua

ukweli kuwa Yesu hakuwa na kosa lolote, lakini bado alimkabidhi ili auawe. Lakini kumbuka, kabla ya Yesu hajapelekwa msalabani, Pilato aliamuru apigwe viboko. Hakuwa na haki ya kufanya hivyo. Katika siku hizo, mtu ambaye aliyesulubiwa hakupaswa kuteswa kabla. Hii haikuwa na ulazima. Lakini alipigwa na maaskari. Injili ya **Mathayo** inatuambia kuwa walichukua fimbo na kumpiga kichwani tena na tena. Nao waliweka na miiba juu ya kichwa chake, na kwamba walikuwa wakichimba ndani ya kichwa chake. Walitumia fimbo ndefu – na katika lile fimbo kulikuwa na vipande vya mfupa na chuma, ili kwamba mgongo wake uchanwe. Misuli yake iliachwa wazi, na nyama yake ilikuwa imechanwa kwa michinjo ya ndani. Watu wengi, walipokuwa wakipigwa namna hii, walikufa kwa sababu ya majeraha yao. Lakini tunaona katika kifungu chetu kwamba, hata baada ya kuwa wamempiga – bado walimtarajia Yesu kubeba msalaba wake mwenyewe, na atembee kupita katika mitaa ya Yerusalemu hadi Golgotha! Alikuwa mdhaifu sana katika hatua hii. Alikuwa karibu na kufa. Na ndiyo sababu askari walilazimika kumtafuta mtu mwingine aubebe msalaba.

Angalia katika **mstari wa ishirini na moja** – na hii inatuleta katika swali letu la tatu. "*Mtu mmoja kutoka Kirene, Simoni baba ya Aleksanda na Rufo aliyekuwa anapita kutoka mashambani, na walimlazimisha kuubeba msalaba*". Je, mtu huyu Simoni ni nani? Tunajua kuwa alikuwa mtu kutoka mji uitwao Kirene, ambao ulikuwa mji muhimu nchini Libya; Afrika Kaskazini. Hivyo, mtu ambaye alibeba msalaba kwa Yesu, alikuwa ni wa Afrika! Pengine alikuwa Myahudi ambaye alikuwa amekuja Yerusalemu kusherehekea Pasaka, na yeye alipoingia katika Yerusalemu, ghafla alilazimishwa kubeba msalaba. Tunajua kwamba alikuwa na wana wawili; mmoja aliitwa Aleksanda na mwingine, Rufo. Inawezekana kwamba huyu ni Rufo yule ambaye Paulo amemtaja katika **Warumi sura ya kumi na sita**, lakini hatuwezi kuwa na uhakika. Pia kuna mapokeo kwamba Simoni wa Kirene aliendelea na kuwa kiongozi katika Kanisa la kwanza, lakini pia, hatujui kama hiyo ni kweli, kwa sababu hatujaambiwa hivyo katika Biblia.

Na hiyo inatuleta kwenye kusulubiwa kwa Yesu juu ya Golgotha; mahali pa fuvu la kichwani; ni kilima kidogo ambacho kilionekana kama fuvu. **Mstari wa ishirini na nne:** "*nao wakamsulubisha*". Askari hao wakainyosha mikono yake. Wakapigilia misumari katika mikono yake, na katika vifundo vya miguu yake - na hapo ndipo pale Yesu alipoangikwa kwa **masaa sita**. Mstari wa **ishirini na tano** unatuambia kuwa ilikuwa ni **saa ya tatu** asubuhi. Marko haitoi maelezo kwa undani zaidi kuhusu mwonekano wa Yesu alipokuwa amesulubiwa, lakini unaweza kuwa na uhakika kwamba, ni mahali pa kutisha kwa watu kuona. Ngoja niwasomee mstari kutoka **Kitabu cha Isaya**. Kumbuka, kitabu hiki kiliandikwa **miaka mia saba** kabla ya Yesu, lakini kwa kweli kinatuambia jinsi kulivyokuwa kusulubiwa kwa Yesu. **Isaya sura ya hamsini na mbili, mstari ya kumi na nne**, inasema hivi: "*Kulikuwa na wengi ambao waliomwona walishangazwa na yeye. Sura yake ilikuwa imeharibiriwa, ilikuwa na damu na kupigwa, zaidi ya sura ile ya mtu yeyote nay a kwamba ilikuwa ni vigumu hata kumtambua kama binadamu*". Je, umewahi kweli kujiuliza juu ya mstari huo? Baada ya kuchapwa na kupigwa, ilikuwa ni vigumu kumtambua Yesu kama alikuwa hata mwanadamu!

Miaka michache iliyopita ilitengenezwa filamu, inayoitwa "*shauku ya Kristo*"; "*mateso ya Kristo*". Baadhi yenu huenda mmeona filamu hii. Watu wengi ambao waliona filamu hii walisema kwamba, ilikuwa ni vurugu na kikatili sana. Ni vigumu kuitazama. Lakini nadhani kwamba filamu hii inaonyesha jinsi ilivyokuwa kwa Yesu. Na bado leo, tunaona michoro mingi ya Yesu ambayo haionyeshi jinsi ilivyokuwa mbaya kwa Yesu msalabani. Kama kijana mdogo nilizoea kwenda kumtembelea bibi yangu - na katika chumba cha kulala kulikuwa na

mchoro wa Yesu kwenye ukuta, na taji la miiba kwenye kichwa chake. Lakini, kulikuwa na mikwaruzo michache tu juu ya uso wake, na matone wachache ya damu yakitiririka chini ya shingo yake. Yesu alikuwa kimya akiangalia juu kuelekea mbinguni. Hivi ndivyo namna picha nyingi zinavyomwonyesha Yesu msalabani. Lakini, sivyo ilivyo kuwa. Kumbuka, kusulubiwa ilikuwa ni njia uchungu sana hadi kufa. Msalaba ulikuwa ishara ya mateso na huzuni, maumivu na vurug

**Mstari wa thelathini na tatu** unatuambia kuwa giza lilikuja juu ya nchi yote, kuanzia **saa ya sita** hadi **saa tisa** mchana. Na kama nilivyosema dakika chache zilizopita kuwa, **mstari wa ishirini na tano** unasema kuwa Yesu alikuwa juu ya msalaba tangu **saa tatu** asubuhi. Je, unaweza kufikiria jinsi ilivyokuwa? Saa sita ni wakati ambapo jua huangaza sana, lakini ghafla kila kitu kiligeuka na kuwa kama usiku! Kuna giza ambalo huifunika nchi yote. Ni lazima lilikuwa ni jambo la kutisha kabisa. Sikiliza mstari huu kutoka Kitabu cha **Amosi**; ni kitabu ambacho pia iliandikwa **miaka mia saba** kabla Yesu. Ni unabii wa leo juu ya msalaba. **Amosi sura ya nane, mstari wa tisa**: *"Katika siku hiyo, asema Bwana mfalme, nitalifanya jua lizimike, na kuitia giza nchi wakati wa mchana".* Hapa katika **Marko sura ya kumi na tano, mstari wa thelathini na tatu**, unabii huu unatimizwa. Hii lilikuwa tendo maalum la Mungu, na ni mojawapo wa miujiza mingi ambayo ilitokea wakati huo.

Kwa nini giza? Kwa nini Mungu alilizimisha jua la katikati ya mchana? Hebu nisome mstari unafuata katika kifungu hicho hicho katika **Amosi sura ya nane**. "*Bwana Mungu anatangaza kwamba, nitaifanya siku hiyo kama siku ya maombolezo kwa ajili ya mwana pekee*". Ikiwa mwana pekee katika familia ya Kiyahudi alifariki, ilikuwa ni siku ya huzuni sana; ni siku ya giza; siku ya huzuni na maombolezo. Fikiria ilivyokuwa ni kama mzazi akimwangalia mtoto wako akisulubishwa. Tunajua kwamba Mariamu, mama wa Yesu, alikuwa amesimama karibu na msalaba wakati Yesu akiwa ameangikwa pale. Je, unaweza kufikiria jinsi Mariamu alivyokuwa? Lakini, hapo msalabani kulikuwa na mzazi mwingine akiangalia tukio hili la kutisha. Kuna mzazi mwingine alikuwa akiomboleza mauaji ya Mwanawe wa pekee; Baba mwenye upendo katika ulimwengu wote. Unamwona, Baba Mungu akiomboleza kifo cha mwanawe mwenyewe; Mungu Baba alikuwepo pale, akiangalia jambo hili likitokea – na hii ndio sababu kulikuwa na giza.

Lakini, si tu kwamba Mungu Baba alikuwa akiangalia tukio hii, yeye mwenyewe alichagua kufanya hivyo! Sikiliza kwa makini sana mstari huu. Barua ya pili ya **Wakorintho, sura ya tano, mstari wa ishirini na moja**, inasema hii. *"Mungu alimfanya yeye asiye na dhambi kuwa mwenye dhambi kwa ajili yetu*." Mungu alimchukua Yesu, ambaye hakuwa na dhambi, na akamwagia dhambi zetu juu yake pale msalabani. Hii ilikuwa hukumu na ghadhabu ya Mungu juu ya dhambi zetu, na ile ilikuwa ni sababu nyingine kutokea kwa giza. Mara nyingi katika Bibilia, tunaona kuwa giza ni ishara ya hukumu. Na alikuwa ni Mungu ambaye aliyafanya haya. Alichukua dhambi zetu, na kuziweka katika mwili wa mwanawe mwenyewe wakati ule alipoangikwa pale juu ya msalaba huo - kwa sababu yeye anatupenda sisi; mimi na wewe.

Je, unaweza kuanza kuyafikiria hayo? Fikiria juu ya dhambi ambazo umezitenda. Matendo na mawazo yako yote mabaya; chuki na dhambi zako zote, na magonjwa – yote yalikuwa juu ya Yesu – katika **masaa sita**! Sasa fikiria juu ya dhambi zote za watu wote wa mji unaoishi. Fikiria juu ya dhambi na uovu katika nchi nzima, na si wakati wa leo tu, lakini kwa maelfu ya miaka. Leta dhambi zote hizo pamoja - dhambi za ulimwengu tangu mwanzo hadi mwisho. Na yote ilimwagwa katika mwili wa Yesu, wakati alipoangikwa pale msalaba. Alikuwa ni

mwana wake mpendwa ambaye alikuwa ametundikwa pale. Kulikuwa ni giza kwa sababu ulikuwa ni wakati wa maombolezo kwa Mungu Baba.

Na katika kipindi hiki cha masaa matatu ya giza, Yesu hakusema chochote; halikutoka neno katika midomo yake. Lakini kuna kitu kingine hapa cha kufikiria; kitu zaidi ya maumivu ya kimwili ya kusulubiwa; kitu zaidi kuliko kubeba dhambi za ulimwengu. Mungu wetu ni Mungu Mtakatifu, na ndani yake hakuna dhambi - na kwa hivyo, Baba wa Mbinguni hangeweza kuwa na uhusiano na Mwanawe Yesu. Baba aligeuza uso wake mbali. Alilazimika kugeuza mgongo wake kinyume na Kristo, na hivyo kwa mara ya kwanza katika historia yote, Yesu alihisi maumivu ya kutengwa na Mungu Baba, na Roho Mtakatifu. Angalia katika **mstari wa thethini na nne.** Ukimya uliendelea kwa muda wa **masaa matatu**, na ghafla, kwa sauti kubwa, Yesu anauvunja ukimya kwa maneno hayo maarufu, kutoka **Zaburi ishirini na mbili, mstari wa moja:** "*Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"*

Na kisha katika **mstari wa thelathini na saba** tunasoma maneno haya: "*Yesu akapaza sauti yake kubwa, akakata roho*". Kwa kweli, katika injili ya **Yohana** tunaambiwa kwamba Yesu alisema: *"Imekwisha*". **Luka** anatuambia kwamba Yesu pia anasema: "*Baba mikononi mwako naiweka Roho yangu".* Ngoja niseme kitu hapa. Yesu hakufa kifo cha kawaida kwa kusulubiwa. Kwa kawaida, mtu aliyesulibiwa, hutokea ukosefu wa nguvu na kushindwa kupumua, kwa polepole alipoteza fahamu na kufa. Na wakati mwingine, ilichukua siku chache kwa mtu kufa msalabani. Lakini, Yesu alikuwa na ufahamu mpaka mwisho. **Yohana** anatuambia kuwa katika dakika hizo za mwisho, Yesu aliinamisha kichwa chake, na kuitoa roho yake. Na kuna mstari wa kuvutia katika **Yohana sura ya kumi** – kabla ya kifo chake, Yesu aliwaambia wanafunzi wake: "*Hakuna mtu atakaye-chukua uhai wangu, lakini ninautoa kwa hiari yangu*." Alikuwa ni Yesu aliyetoa roho yake. Aliamua wakati gani ulikuwa ni wakati wa kufa. Maisha yake hayakuchukuliwa kutoka kwake; yeye aliyatoa maisha yake kwa hiari yake.

Na wakati huo wa kifo, wakati Yesu alipoyatoa maisha yake, na kukata roho, angalia kile kinachotokea katika **mstari wa thelathini na nane**: "*pazia la Hekalu lilipasuka vipande viwili, kutoka juu hadi chini". Nini* maana ya muujiza huu? Katika Hekalu, kulikuwa na pazia hili kubwa, ambalo lilipatengaisha mahali Patakatifu pa Patakatifu, na uwanda wa makuhani. Hakuna mtu ambaye angeweza kuingia sehemu hiyo. Ilikuwa ni marufuku. Mara moja tu kwa mwaka, kuhani mkuu aliruhusiwa kuingia katika chumba hiki - katika Siku ya Upatanisho. Kuhani alienda humo kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi za watu. Lakini sasa, pazia hili kubwa lilikuwa limekatwa na Mungu! Je, Mungu anasema nini hapa? Kwanza kabisa, Mungu alikuwa akisema kwamba, dhabihu za wanyama zilikuwa hazi-hitajiki tena. Kamwe kuhani hakuwa na haja ya kwenda katika Patakatifu pa Patakatifu, ili kutoa sadaka. Kwanini? Kwa sababu Yesu alikuwa dhabihu kuu kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Pili, sikiliza mistari hii kutoka **Waebrania sura ya kumi, mistari ya kumi na tisa, na ishirini:** "*Sasa tunaweza kupaingia kwa ujasiri mahali patakatifu pa mbinguni, kwa sababu ya damu ya Yesu. Hii ni njia mpya, iliyo hai tuliyofunguliwa kupitia lile pazia takatifu, kwa njia ya kifo chake kwa ajili yetu. Kwa kuwa tunaye Kuhani Mkuu, ambaye anatawala juu ya watu wa Mungu, basi tumkaribie Mungu kwa moyo was kweli na imani Timilifu".*

Kwa maneno mengine, mbingu iko wazi, kwa wote ambao wamechagua kuchukua kimbilio katika Kristo, na tunaweza kuja katika uwepo wake Mtakatifu, si mara moja tu kwa mwaka katika tukio maalum, lakini wakati wowote tunaopenda - kwa sababu tu ya kile ambacho Kristo amekifanya juu ya msalaba. Pia ina maana kwamba hatuna haja ya kupitia kwa mtu

mwingine; hatuhitaji kutubu dhambi zetu kwa kuhani, kama wanavyofanya katika Kanisa Katoliki. Tunaenda kwa moja kwa moja kwa Mungu kupitia maombi. Yeye peke yake ndiye Kuhani Mkuu, na Mpatanishi wetu. Yeye peke yake ana uwezo wa kusamehe dhambi. Habari mbaya ni hii. Nadhani makuhani walilitengeneza tena pazia, na kulirudisha mahali pake katika nafasi yake - ili patakatifu pa patakatifu pazuiliwe tena. Ni huzuni kiasi gani, wakati Kristo amefungua njia kwenda kwa Mungu – lakini watu wanachagua kuweka pazia ili kuziba tena. Mara nyingi hutokea hata leo. Pazia imeondolewa, lakini dini mara nyingi hutafuta kulirudisha pazia tena, na kutaka kuaminisha kwamba uhusiano na Mungu Mtakatifu hauwezekani, mpaka tuweze kuishi kwa njia fulani. Habari njema ni kwamba tunaweza kwenda jinsi tulivyo; watu wenye dhambi. Tunaweza kwenda ndani ya pazia, kukiri na kutubu dhambi zetu, kutafuta msamaha wake. Na kwa sababu ya msalaba *"Yeye ni mwaminifu na wa haki, na atatusamehe dhambi zetu"* (1 Yohana 1:9).

Angalia mstari wa mwisho katika kifungu chetu. **Mstari wa thelathini na tisa**: “*Hakika mtu huyu bila ya shaka ni Mwana wa Mungu*.” Na Mkuu wa Kirumi ambaye alisimama karibu na msalaba, alipoona kile kinachotokea kwa Yesu, alisema: “*hakika mtu huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu*”. Je, mtu huyu alifanyika kuwa muumini? Hatujui. Hatujui kile kilichomtokea – labda aliamini. Huenda alifanyika kuwa Mkristo, na kujiunga na Kanisa la kwanza huko Yerusalemu. Nina matumaini kwamba, tunapoukumbuka msalaba, na kama sisi tukisimama chini ya msalaba, tunaweza kusema kwa pamoja na huyu Mkuu wa Kirumi, “*hakika, Yesu alikuwa Mwana wa Mungu, ambaye alikufa kwa ajili yetu*”.

-----------------------------------------